



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA SONGWE



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na.SDC /A.20/16/56

Tarehe: 09/06/2023

TANGAZO LA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Songwe anapenda kuwatangazia watanzania wote wenye sifa na nia ya kufanya kazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Songwe kuomba nafasi zifuatazo.

MTENDAJI WA KIJIJI – NAFASI MBILI (2)

SIFA

Awe na Elimu ya Kidato IV-VI aliyehitimu mafunzo ya Astashahada / Cheti katika moja ya Fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo au chuo chochote kinachotambulika na Serikali.

KAZI NA MAJUKUMU

- Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji.
- Kusimamia Ulinzi na Usalama wa Raia na mali zao, kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala bora katika Kijiji.
- Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa mpango wa maendeleo ya Kijiji.
- Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
- Kutafsiri na Kusimamia Sera, Sheria na Taratibu.
- Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza Mikakati ya kuondoa njaa, Umasikini na kuongeza uzalishaji mali.
- Klongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaalamu katika Kijiji.
- Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji.
- Mwenyekiti wa Kikao cha Wataalamu waliopo katika Kijiji.
- Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya Wananchi.
- Kusimamia utungaji wa Sheria ndogo za Kijiji.

**NGAZI YA MSHAHARA – TGS B
MASHARTI YA UJUMLA**


- Mwombaji awe Mtanzania mwenye umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45.
- Mwombaji aambatanishe Cheti cha kuzaliwa.
- Mwombaji aambatanishe maelezo yake binafsi yaliyojitosheza (CV) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika pamoja na namba zao za simu.
- Maombi yaambatanishwe na picha moja (Passport size) ya hivi karibuni na iandikwe jina kwa nyuma.
- Barua za maombi ziandikwe kwa mkono na ziambatanishwe na nakala za vyeti vya Elimu na taaluma kutoka vyuo vinavyotambuliwa na Serikali.
- Testimonials, Provisional results, Statement of results hazikubaliki.
- Waombaji wote ambao wamesoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vimefanyiwa ulinganishi na TCU na NACTE.
- Waombaji wote watapaswa kuangalia mara kwa mara kwenye tovuti ya Halmashauri kwani wale watakaoitwa kwenye mchujo wa awali majina yatawekwa hapo.
- Maombi yote yatumwe kama njia ya Posta kwa anuani ifautavyo.

Mkurugenzi Mtendaji (W),
Halmashauri ya Wilaya ya Songwe,
S.L.P 77

MKWAJUNI- SONGWE


Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 23/06/2023 saa 9.30 Alasiri,
Imetolewa na:

N.B. Tangazo hili linafuta tangazo Kumb.Na.SDC/20/16/55 la tarehe 01/06/2023.


Abdallah Mgobja

KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA

Nakala: Katibu


MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA
SONGWE

Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma,
Jengo la Utumishi (UDOM)
Eneo la Dkt Asha Rose Migiro,
Sanduku la Posta 2320

DODOMA

Tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Songwe www.songwedc.go.tz
Tovuti ya Sekretarieti ya Ajira www.ajira.go.tz
Mbao za Matangazo – Kata zote za Halmashauri ya Wilaya ya Songwe